**3061**
**BUSINESS KISWAHILI**
**STAGE III**
**July 2007**
**Time: 3 hours**

MANYAM FRANCHISE
Discover!Learn!Apply

## THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

## BUSINESS EDUCATION SINGLE AND GROUP CERTIFICATE EXAMINATIONS

BUSINESS KISWAHILI
STAGE III

**3 hours**

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA**

*Jibu maswali **YOTE**.*
*Jibu maswali kikamilifu.*

**This paper consists of 11 printed pages**

**Candidates should check the question paper to ascertain that all the pages are printed as indicated and no questions are missing.**

© 2007 *The Kenya National Examinations Council*

Powered By: www.manyamfranchise.com

1. *Soma kifungu kifuatacho cha maneno, kisha ujibu maswali yatakayofuatia.* (Alama 18)

Miaka mingi imepita tangu mataifa mengi ya Kiafrika kujinyakulia uhuru wao. Wananchi wa mataifa haya walimpinga mkoloni wakifikiria kuwa baada ya mkoloni kuondoka wangeziendeleza nchi zao vyema kiuchumi. Migogoro ya kila aina ilizuka na vita vikashamiri. Mkoloni alikuwa hana budi ila kuondoka katika mataifa haya ya Kiafrika. Basi sherehe za kuzikabidhi nchi uhuru zikafanywa lakini punde si punde mataifa haya yakagundua kuwa ingawa mkoloni alikuwa ameondoka, athari zake zilihisika kwa njia namna namna. Walibaini kuwa, uhuru walioupenda ulikuwa ni wa bendera tu. Walihisi hivyo kwa kuwa wakoloni waliendelea kuzitawala nchi hizi kiuchumi wakiwa mbali. Ukoloni huu mpya ukaitwa ukoloni mamboleo na ule wa mbeleni ukawa ndio ukoloni mkongwe.

Matokeo ya aina hii mpya ya ukoloni yakawa ni kuibuka na kuimarika kwa matabaka mawili makuu: tabaka la juu ambalo lilijumuisha viongozi na matajiri wa mataifa haya na tabaka la chini ambalo lilikuwa ni la wananchi wachochole. Viongozi na matajiri hawa wakaiga tabia za wakoloni na wakaanza kuziendeleza katika nchi zao. Wakaimarisha uhusiano wa karibu na watawala wao wa zamani na wakaendeleza ukoloni - mamboleo kwa njia nyingi. Wakaanza kujinyakulia ardhi na mali ambayo ingemilikiwa na mafukara. Wakajijengea majumba makubwa ya kifahari katika sehemu za mijini na kwingineko. Majumba ya ziada yakawa wanayapangisha kwa watu mbalimbali na matajiri wakazidi kujilimbikizia mali. Wengi wa viongozi hawa wakaomba misaada kutoka kwa wakoloni na kuanzisha mashirika mbalimbali nchini wakiwa na lengo la kujizalishia mali nyingi. Wakawaajiri wenyeji wao na **kuwapa ijara duni** ambayo ingewawezesha kujiruzuku kibaba tu. Waajiriwa wakazidi kuumia hata wasiweze kujidundulizia pesa kidogo na kujiwekea akiba.

Matajiri hawa baada ya kupata mali nyingi wakaitumia na kuweka akiba zao katika nchi za nje badala ya kuzitumia katika kuendeleza mataifa yao. Mataifa ya kimagharibi yakawa yanafaidika kutokana na riba ya pesa hizo zilizohifadhiwa katika benki zao. Nchi za Kiafrika zikaendelea kuzama katika lindi la ulitima. Tabaka hili la juu likabaki kuwa tabaka lililojiimarisha kwa kila njia. Wakwasi hawa wakawa wanawapeleka wana wao kusomea katika nchi za ng'ambo; wakawa wanatumia pesa nyingi kwa malipo ya karo katika vyuo mbalimbali vya ng'ambo.



Powered By: www.manyamfranchise.com

Jambo la kusikitisha likawa ni kuwa wengi wa wana hawa walihiari kuajiriwa huko ng'ambo baada ya kukamilisha masomo yao badala ya kurejea nchini mwao na kusaidia katika ujenzi wa taifa. Wakaendelea kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi hizo. Matajiri hawa wakajitenga na ulitima unaowapa Waafrika wenzao **adha za kila nui**. Wakawa wanachoma pesa kwa kukaa sehemu zilizo na maisha ya hali ya juu na ghali huku wakijitenga na kusahau ujenzi wa taifa lao.

Watu wa tabaka la chini, nao wakawa wanaishi katika hali duni kiuchumi na kimazingira. Kuna wale walioishi katika sehemu za mabanda, huku wengine wakiishi vichochoroni, mbingu zikiwa ndizo paa, siku nenda siku rudi. Wachochole hawa wakawa hata hawajui utamu wa godoro kwa kuwa walilalia ardhi. Wengi wao wakakonda mithili ya ng'onda kwa kujisaga mchana kutwa wakifanya kazi za sulubu zenye malipo haba. Wengine wao wakakata kamba kwa ukosefu wa mahitaji muhimu kama vile chakula na matibabu. Matibabu yakawa ni kwa wale walioweza kuyalipia. Isitoshe, waliosalia, wengine wao wakakosa elimu na libasi bora. Bila elimu viokote hawa wakaendelea kukosa kazi za ajira bora na ukata usiokadirika ukaendelea kushamiri miongoni mwa kina yahe.

Ukosefu wa wananchi walioelimika vya kutosha ukaipelekea Serikali husika kuagiza wataalamu kutoka nchi za nje ili waje kuzifanya amali ambazo zingeweza kutekelezwa na Waafrika wenyewe. Serikali husika iliwalipa wataalamu hawa mishahara ya juu sana. Viongozi wa nchi za Kiafrika walitumia pesa nyingi kuwakuza kwa njia nyingi. Mathalani, mhandisi wa kizungu huku Afrika akawa analipwa ujira mkubwa zaidi akilinganishwa na mhandisi Mwafrika hata ingawa walifanya kazi zilizolingana. Mwajiriwa huyu mzungu alipoajiriwa na nchi-husika alipewa boi wa nyumba, yaya wa kutunza watoto wake na isitoshe, akawa anapewa mtumishi mwingine wa kutunza bustani na wa kumlimia kikataa iwapo alikuwa nacho. Aidha mwajiriwa huyu alipewa **bahari ya nyumba** iliyogharamiwa na Serikali ya nchi-husika na akaendelea kufurahia uchumi wa mataifa ya Kiafrika huku Waafrika waliozifanya kazi zizo hizo wakipewa vijumba bila huduma za ziada.

Hata hivyo, wakoloni wengine walianzisha na kuimarisha uhusiano wa kibiashara na baadhi ya viongozi wa nchi za Kiafrika. Wakuu hawa wa nchi za Kiafrika wakawapa nafasi ya kuingia katika nchi zao kama wawekezaji. Wakajenga na kuanzisha viwanda vya utengenezaji wa bidhaa mbalimbali. Mfano wa viwanda kama hivyo ni kile cha ushonaji nguo cha EPZ huko Athi River. Kiwanda kama hiki hufaidika sana kwani wamilisi wanapata malighafi kwa gharama ya chini. Pia wanawafanyiza wananchi kazi nyingi kwa malipo duni sana. Nguo



Powered By: www.manyamfranchise.com

zinazotengenezwa katika kiwanda hicho hupelekwa katika mataifa ya kimagharibi na kuwekwa chapa za nchi hizo za ng'ambo. Baada ya hapo bidhaa hizo hizo huuzwa tena katika mataifa ya Kiafrika kwa bei ghali sana. Jambo hili linamaanisha kuwa, wanaonufaika ni mataifa ya nje, huku nchi za Kiafrika zikiendelea kunyanyaswa. Ni dhahiri shahiri kuwa wafanyikazi wa kizungu wanaofanya kazi katika viwanda kama hivi hulipwa mishahara mikubwa kuliko wenyeji. Wafanyikazi hawa wazungu huhifadhi pesa zao katika benki za huko kwao na kujiendeleza kiuchumi. Katika mataifa yaya haya ya Kiafrika, wakoloni wengine zaidi walirudi kwa 'hila' na kujitahidi kwa udi na uvumba kuwa na urafiki na viongozi wa nchi hizi. Hawa walijifanya kuwa wao ni wafanyibiashara mashuhuri wenye nia ya kusaidia kuimarisha uchumi wa nchi hizi. Wao huziahidi nchi hizi kuwa watatumia pesa zao kugharamia miradi ya kimaendeleo lakini hawatimizi ahadi hiyo. Waafrika walisahau kuwa bure yaumiza. Basi wafanyibiashara hawa waliwafumba macho viongozi na kwa hila hata wakahepa malipo ya ushuru wa forodhani. Wakaagiza na kuingiza nchini bidhaa zao za biashara bila malipo yoyote. Wakauza bidhaa hizi kwa bei ghali na kufaidika si kidogo. Walikuwa wanafahamu kinagaubaga kuwa watakapofanikiwa kwa yaliyowaleta katika nchi hizi, watarejea kwao na vibindo vya pesa kuchangia ustawi wa uchumi wao. Nchi za Kiafrika zinaendelea kuzoroteka kiuchumi kwani huchukua muda kuutambua ujanja wa wakoloni wakongwe.

Pia ni dhahiri kuwa baada ya uhuru, mataifa yaliyozitawala nchi hizi, yaliendelea kuutawala uchumi wa nchi husika kupitia mashirika ya fedha kama vile, Shirika la Fedha la Dunia (IMF) na lile la Benki Kuu ya Dunia (W.B.) na mengineyo kama yale yanayoamua bei za bidhaa katika kiwango cha dunia. Kwa kuwa nchi nyingi za bara la Afrika zilikuwa zimelemewa na umaskini, zilianza kuyategemea mashirika haya kwa misaada ya kifedha. Mashirika haya yakawa yanawapa misaada ya kifedha kwa masharti magumu. Kwa mfano, nchi ya Kenya iliwekewa masharti magumu kama vile kulazimishwa kupunguza idadi ya wafanyikazi wa Serikali, kubadilisha mfumo wa elimu na kutakiwa kuanzisha mfumo wa kisiasa wa vyama vingi. Kwa kutokuwa na la kufanya, Kenya ilikubaliana na masharti hayo huku ikifahamu kuwa masharti haya yangewaumiza wananchi wake. Pamoja na mchango wao wa kutoa misaada ya kimaendeleo, masharti hayo ndiyo yanayoiamulia Afrika, mambo mengi kama vile bei za bidhaa zinazozalishwa nchini na mazao yanayouzwa katika soko la dunia kwa mfano kahawa, katani, pamba, pareto, chai na nyinginezo! Uamuzi wao aghalabu huwa wa kuteremsha bei za mazao na bidhaa zinazopatikana barani Afrika na wakati huo huo wanapandisha bei za bidhaa zao ambazo hutoka viwandani mwao. Hizi ni bidhaa kama vile magari na mashine mbalimbali.



Powered By: www.manyamfranchise.com

Jambo la kusikitisha na kukata ini ni kwamba idadi kubwa ya nchi za Kiafrika zinahitaji misaada hii ya kifedha ili ziendelee kujiimarisha kiuchumi kulingana na takwimu, tisaini kwa mia ya bidhaa za nchi zinazoendelea hununuliwa na nchi za kigeni kwa bei che, hivyo basi nchi hizo za kigeni huendelea kujinufaisha.

Hata hivyo, **miale ya mapambazuko ya ufahamu** kwa Waafrika kuwa wanadhulumiwa na mataifa yaliyoendelea imeanza kudhihirika miongoni mwa viongozi wengine wa nchi hizi. Baadhi ya viongozi wa nchi hizi za kiafrika wamekuja kutambua kuwa, kupokea misaada ya kila aina kutoka mataifa yaliyoendelea ni kuyafanya mataifa yao yaendelee kuyategemea mataifa ya Ulaya.

Jambo ambalo linaweza kuzisaidia nchi hizi ni kuwa na uwezo wa kurekebisha baadhi ya vile vikwazo vilivyowekwa na nchi zilizoendelea kuhusu bidhaa zinazoingia katika nchi zao, kwa mintarafu ya ushuru wa forodha. Kwa mfano, Marekani inatoza ushuru wa asilimia ndogo kwa ndizi zilizokaushwa na asilimia kubwa kwa unga wa ndizi unaoingia nchini mwao ilhali ndizi katika hali ya kawaida hazina ushuru wowote. Jambo la kushangaza ni kwamba bidhaa kama vile mbao, pamba na madini kama vile dhahabu, fedha na mengineyo, hayatozwi ushuru lakini bidhaa zake kama vile pete, makasha na samani hurudi Afrika zikiwa zinauzwa kwa bei ghali. Haya maelezo yanamaanisha kuwa, mataifa yaliyoendelea, yataendelea kunufaika kwa malighafi, zinazoingizwa nchini mwao ilhali mataifa ya Kiafrika yataendelea kuzoroteka kwa kununua bidhaa zinazotokana na vitu hivyo vyao kwa bei ghali.

(a) Eleza tofauti kati ya ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. (Alama 2)

(b) Kuwepo kwa uhusiano wa karibu kati ya viongozi wa Kiafrika na wakoloni wao wa zamani kuna hatari gani kulingana na taarifa uliyoisoma? (Alama 2)

(c) Jadili jinsi mataifa ya Kiafrika yanavyoweza kujikomboa kutokana na swala la ukoloni mamboleo. (Alama 3)

(d) Kulingana na makala uliyosoma, ni kwa vipi tunaweza kudai kuwa vya bure vinaweza kuumiza bara la Afrika? (Alama 3)

(e) Kwa kurejelea taarifa uliyosoma, onyesha jinsi Shirika la Fedha la Dunia na lile la Benki Kuu ya Dunia yanavyochangia kuzorotesha uchumi katika mataifa ya Kiafrika. (Alama 4)



Powered By: www.manyamfranchise.com

(f) Eleza maana ya vifungu vya maneno vifuatayo kama vilivyotumiwa katika taarifa. (Alama 4)

(i) kuwapa ijara duni;

(ii) adha za kila nui;

(iii) bahari ya nyumba;

(iv) miale ya mapambazuko ya ufahamu.

2. *Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yatakayofuatia.* (Alama 18)

Ufugaji in mojawapo ya aina za kilimo. Hii ni shughuli muhimu na kuu miongoni mwa jamii zinazoishi katika sehemu zenye mvua nyingi na pia sehemu kame. Sekta hii iko chini ya Wizara ya Ustawi wa Mifugo na Uvuvi. Wizara hii huwa na jukumu la kusimamia na kushirikisha uzalishaji wa mifugo na umarishaji wa uvuvi kwa maendeleo ya taifa letu.

Kulingana na takwimu sekta ya ufugaji huchangia asilimia kumi ya jumla ya mapato ya nchi (GDP) na inasimamia zaidi ya asilimia thelathini ya thamani ya mazao ya kilimo shambani.

Hata hivyo, maeneo yenye mvua nyingi kama vile, sehemu za Mkoa wa Kati na zingine za Mkoa wa Bonde la Ufa hufuga mifugo wanaotoa maziwa kwa wingi. Wenyeji wa sehemu kame kama vile Mkoa wa Kaskazini Mashariki na sehemu zingine za Mkoa wa Bonde la Ufa kama Wilaya ya Kajiado na kwingineko huendeleza kilimo hiki cha ufugaji. Sehemu hizi kame ni maarufu kwa utoaji wa nyama kwa wingi. Zaidi ya asilimia sitini ya mifugo wote wa Kenya hutoka katika sehemu hizi kame na huajiri asilimia tisini ya wenyeji. Iwapo serikali ingejenga kiwanda cha kuuza mifugo katika Mkoa wa Kaskazini Mashariki, ingesaidia sana kuimarisha maisha ya wenyeji na pia kuongezea pato kwa nchi kutokana na Sekta ya Ufugaji. Wananchi wangeweza kuuza mifugo wao kwa njia rahisi kwani hawatalazimika kuwapakia katika malori ili wasafirishwe hadi kiwanda cha KMC huko Athi River. Kiwanda cha aina hiyo kikijengwa katika sehemu hizo za Mkoa wa Kaskazini Mashiriki, Serikali itakuwa haina budi kuimarisha njia za mawasiliano. Pia itahakikisha kuwa kuna maji ya kutosha katika sehemu hizo kwani maji ni muhimu sana katika uendeshaji wa viwanda. Sehemu hizo zitaweza kunawirika na kuvutia sana. Watalii wataweza kuzitembelea na bila shaka, serikali itaweza kujipatia pesa za kigeni kutokana na ziara za watalii hawa.



Powered By: www.manyamfranchise.com

Isitoshe, nchi inaweza kunufaika kutokana na sekta ya ufungaji ambayo huweza kuiletea nchi pesa za kigeni kupitia mauzo ya wanyama walio hai, ngozi zao na bidhaa za maziwa. Pia isisahaulike kuwa sekta hii huajiri asilimia hamsini ya wafanyikazi katika sekta ya kilimo. Ufungaji huchangia pakubwa kwa mapato ya familia kupitia mauzo ya mifugo na bidhaa za mifugo hao. Hizi huwa ni bidhaa kama vile mafuta, maziwa na ngozi. Kutokana na mauzo hayo familia huweza kujikimu na kujiendeleza kimaisha. Fauka ya haya, sekta hii hutoa malighafi kwa viwanda vinavyohusiana na kilimo, kama vile kiwanda cha maziwa cha KCC na vinginevyo. Wakulima wafugaji huuza maziwa yao katika viwanda kama hivi na kupata faida. Wengine wao huweza kutajirika kwa njia hiyo hata huweza kuanzisha miradi ya kimaendeleo mumu humu nchini. Matajiri hawa husaidia katika kupunguza tatizo sugu la ukosefu wa kazi na ulitima humu nchini kwa kuajiri baadhi ya wananchi.

Sekta ya ufungaji wa ng'ombe wa maziwa huchangia asilimia themanini na nane (88%) ya jumla ya maziwa yanayohitajika nchini. Ngamia nao huchangia kwa kutoa asilimia tisa za maziwa, nao mbuzi asilimia tatu. Kulingana na takwimu, maziwa huchangia asilimia tatu nukta tano (3.5%) ya jumla ya mapato ya nchi (GDP) na asilimia kumi na nne (14%) ya kilimo kwenye mapato ya jumla ya kitaifa. Kenya ni nchi inayojitosheleza kwa maziwa na bidhaa zinazotokana na maziwa hayo. Tatizo hutokea tu wakati wa hali mbaya ya anga. Ng'ombe wengi huathirika na hata kufa. Ni muhimu kukumbuka kuwa, bidhaa zinazotokana na ng'ombe wa maziwa ni muhimu kwa uchumi wa nchi.

Hata hivyo, uzalishaji wa maziwa na nyama ya ng'ombe umekuwa ukipungua kutokana na ukame wa muda mrefu, huku wateja wake wakiendelea kuongezeka. Inafaa washikadau wote katika sekta hii kushirikiana katika kukabiliana na upungufu huo ili kuweza kuendelea kutimiza mahitaji ya kitaifa na kuweza kuuza bidhaa za ziada katika nchi za kigeni. Inakadiriwa kuwa, kila mwaka, tani elfu mia tatu na arobaini za nyama huzalishwa humu nchini na zitazidi kuimarishwa kwa sababu ya ufunguzi wa kiwanda cha nyama cha Athi River.

Tatizo hili la ukame wa muda mrefu limeathiri sana sekta hii ya ufugaji. Ilibidi Serikali ya Kenya kukabiliana na swala la kiangazi cha muda mrefu ambacho kilileta hasara kubwa kwa wafugaji na nchi kwa ujumla. Maelfu na maelfu wa mifugo waliangamia. Serikali ilikuwa



Powered By: www.manyamfranchise.com

haina budi ila kuchukua hatua kabambe kukabiliana na janga hilo. Ilitoa kwa dharura shilingi milioni mia nne za kununua mifugo wengine, kugharamia chanjo na pia kununulia dawa za minyoo kwa mifugo waliosalia, pia sehemu ya pesa zizi hizi zilitumiwa katika ununuzi na usambazaji wa nyasi katika maeneo yaliyokumbwa na ukame.

Shughuli hii ilisimamiwa na wizara hii ya ufugaji ikishirikiana na Shirika la Ustawi wa Kilimo (ADC) na lile la Kifedha la Kilimo (AFC). Kufikia sasa ng'ombe wengi wamenunuliwa na kuhifadhiwa katika mashamba kwa matunzo. Serikali pia imechukua hatua ya kutoa mafunzo kwa wafugaji na wakulima. Mafunzo haya yatawawezesha kubashiri mapema hali ya anga na kuchukua hatua mwafaka katika kukabiliana na hali yoyote ya anga.

Ili kuimarisha uzalishaji na upanuzi wa biashara ya mifugo na bidhaa zake, Serikali inajitahidi kutenga maeneo mahsusi yanayofaa kwa ufugaji bora na kufanya utafiti wa kupata njia bora za kudhibiti magonjwa. Aidha Serikali imejitolea mhanga kuchunguza sana ripoti zozote za kuzuka kwa magonjwa mbalimbali. Yanapopatikana Serikali huchukua hatua mara moja na kudhibiti usafirishaji wa mifugo kutoka sehemu moja hadi nyingine. Pia inaendelea kutoa chanjo dhidi ya magonjwa sugu ambayo huweza kuathiri biashara ya mifugo pamoja na bidhaa zake. Aidha Serikali huhakikisha kuwa mifugo wamepitishwa kwenye majosho ili kukingwa kutokana na magonjwa mbalimbali. Kuna magonjwa mengine ambayo hata huweza kuathiri uzalishaji wa mifugo na kusababisha hasara isiyokadirika kwa nchi. Kulingana na utafiti uliofanywa, imegunduliwa kuwa asilimia sitini ya maeneo yenye umajimaji yamejaa mbung'o ambao huwang'ata wanyama hawa. Ili kuwakinga wanyama hawa dhidi ya wadudu hawa, Serikali hunyunyizia dawa umajimaji huo na kuubadilisha sehemu hizo kuwa mabwawa bora ya kusaidia wanyama hasa nyakati za ukame.

Aidha sekta nyingine ya ufugaji na ambayo huchangia kwa kiasi fulani ustawi wa uchumi katika nchi ni ile ya uvuvi. Sekta hii huchangia asilimia nukta tano (0.5%) ya jumla ya mapato ya nchi. Katika mwaka wa 2004, jumla ya tani 134,000 za samaki wenye thamani ya shilingi bilioni nane zilizalishwa hapa nchini. Mauzo ya samaki katika nchi za kigeni mwaka huo yaliletea nchi yetu faida ya shilingi bilioni tano.

Uvuvi hutegemewa na watu elfu themanini moja kwa moja kwa chakula. Watu elfu mia nane kwa njia moja au nyingine hufaidika kutokana na uvuvi. Kwa wengine uvuvi ni kazi inayowawezesha kupata kipato kikubwa.



Powered By: www.manyamfranchise.com

Ili sekta hii ya ufugaji iimarike na iweze kuchangia pakubwa zaidi katika maendeleo ya uchumi wa nchi ni muhimu kwa Serikali kuimarisha maeneo ya samaki kama vile, ziwa Turkana na mito mbalimbali kama vile, ule wa Tana River na mingineyo. Pia Serikali inapasa itoe mikopo kwa wavuvi ili waweze kupanua biashara zao na kuchangia zaidi maendeleo katika taifa letu. Kuna pia ufugaji wa nyuki ambao unakua kwa kasi sana. Ufugaji huu husaidia watu wengi kurina asali kwa wingi. Kutokana na mauzo ya asali nchini na katika nchi za ng'ambo, watu huweza kupata donge nono la kukidhia haja zao. Isitoshe, wataweza kuchangia katika uimarishaji wa uchumi wa nchi.

Kuna mashirika ya kibinafsi, yasiyo ya Kiserikali ambayo huwasaidia wananchi kuimarisha kilimo cha ufugaji wa nyuki. Baadhi ya Mashirika haya ya Kibinafsi ni Shirika la Kimataifa la 'Africa Now'. Shirika hili hudhamini miradi ya ufugaji wa nyuki katika Mkoa wa Nyanza na wa Magharibi. Kwa msaada wa shirika hili, watu wengi wamejiunga na kilimo hiki cha ufugaji nyuki. Uzuri wa ufugaji wa nyuki ni kwamba hauhitaji kiasi kikubwa cha fedha na nyuki hustahimili hali zote za hewa.

Shirika jingine ni la 'Honey Care'. Hili huwasaidia wafugaji wa nyuki kwa kuwatengenezea na kuwasambazia mizinga na vifaa vya kurina asali. Kila mojawapo ya mizinga hii huweza kuzalisha kati ya kilo kumi na kumi na tano za asali. Asali hii huvunwa mara tano kwa mwaka na kuwafaidisha wahusika. Shirika hili la 'Honey Care' limeanzisha kilimo cha ufugaji wa nyuki wilayani Mwingi, Makueni, Kitui, Taita na Voi. Asali katika sehemu hizi hupatikana kwa wingi na sasa kuna watu wengi wanaofanya biashara za kuuza asali hapa nchini na hata katika nchi za nje. Kutokana na mauzo ya asali, watu huweza kuzikimu familia zao kistahiki. Wengine hutumia pesa wanazopata kuwaelimisha watoto wao hadi vyuo vikuu vya mumu humu nchini na kwingineko. Katika wilaya ya Makueni huko Kibwezi, baadhi ya wafugaji wamejijengea viwanda vidogo vidogo vya kutengenezea asali. Viwanda hivi huajiri baadhi ya wenyeji wa sehemu hiyo na kuwanufaisha mno.

Ni muhimu kwa serikali kuwatambua wakulima wafugaji hawa na kuwapa mikopo ili waendelee kujiimarisha na kuviimarisha viwanda vyao kwa maendeleo ya taifa letu.

(a) Eleza jinsi sekta ya ufugaji na uvuvi inavyochangia katika kuimarika kwa uchumi wa taifa letu (Tumia maneno 80 - 90) (Alama 6)

(b) Jadili matatizo mbalimbali yanayoathiri sekta ya ufugaji na uvuvi, kama yalivyoelezwa katika taarifa uliyoisoma. (Tumia maneno 55 - 60) (Alama 4)



Powered By: www.manyamfranchise.com

(c) Onyesha hatua ambazo zimechukuliwa na serikali katika harakati za kuimarisha sekta ya ufugaji (Tumia maneno 100 - 110). (Alama 8)

3. *Andika insha juu ya:* (Alama 22)

(a) Umesoma katika gazeti la BARAZA tangazo kuwa wanafunzi waliohitimu mafunzo ya uhazili katika vyuo mbalimbali vya humu nchini, wanatakikana katika matawi mbalimbali ya Benki ya 'Maarifa': Kuna nafasi za kazi za wahazili. Andika barua kwa mkurugenzi wa benki hiyo uombe kazi hiyo. (Alama 11)

(b) Baadhi ya wafanyikazi wana tabia za kuchuuza katika ofisi. Wewe kama Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la PONGEZI, waandikie arifa uwaonye dhidi ya tabia hii. (Alama 11)

4. (a) Soma jedwali lifuatalo ambalo linaonyesha makadirio ya kibinafsi ya matumizi ya mshahara wa Jeni kwa muda wa miezi mitatu mtawalia, kisha ujibu maswali yanayofuata.

| | JANUARI | FEBRUARI | MACHI |
|---|---|---|---|
| Malipo | Sh. 25,000 | Sh. 25,000 | Sh. 25,000 |
| Matumizi | | | |
| Chakula | Sh. 3,000 | Sh. 3,500 | Sh. 4,100 |
| Nyumba | Sh. 8,000 | Sh. 8,000 | Sh. 8,000 |
| Nguo | Sh. 4,500 | - | Sh. 3,000 |
| Viatu | Sh. 1,000 | Sh. 1,500 | - |
| Nauli | Sh. 3,000 | Sh. 3,000 | Sh. 3,000 |
| Matumizi ya Jumla | Sh. 19,500 | Sh. 15,000 | Sh. 18,100 |

(i) Taja jumla ya pesa alizoweza kuzitumia Jeni kwa chakula kwa muda huo wa miezi hiyo mitatu. (Andika jawabu kwa maneno). (Alama 1)

(ii) Ni miezi gani ambayo Jeni hakuweza kununua baadhi ya vitu vilivyo katika makadirio ya pesa zake? (Alama 2)

(iii) Katika mwezi wa Fabruali Jeni alijiwekea akiba ya kiasi gani cha pesa za mshahara wake? (Andika jawabu lako kwa maneno). (Alama 1)

(iv) Andika asilimia ya kiasi cha pesa kilichotumiwa katika ununuzi wa nguo kwa muda huo wa miezi mitatu. (Alama 2)



Powered By: www.manyamfranchise.com

(b) Kwa kutumia maneno 250, eleza vile Serikali inavyoweza kuwashirikisha watoto wa mitaani katika ujenzi wa taifa letu. (Alama 10)

5. Barua ifuatayo imeandikwa na mfanyi biashara mwenye kitembo cha chini cha elimu kwa Meneja Mkurugenzi, Benki ya Biashara, tawi la Kitale. Iandike upya usahihishe makosa ya kimuundo. (Alama 14)

Bwana,

Kuh: Mkopo wa shilingi milioni moja.

Tarehe 10.09.2005

S.L.P. 242
Kitale

Mkopo ninaouomba utalipwa kwa kipindi cha miaka minne. Watu wafuatao wamekubali kuwa wadhamini wangu:

1. Bw. Juma Njuguna,
S.L.P. 104
Kitale.

2. Bw. Karanja Kamau
S.L.P. 183
Mkuu wa Wilaya
Kitale.

Wako mwaminifu,
John Tumaini
JTumaini

Natumaini ombi langu litafikiriwa.

Mimi ni mfanyibiashara na nina mikahawa mingine mitatu huko Mombasa na mingine miwili Nairobi. Pia nimejenga majumba matatu ya aushi ya kukodisha kule Nakuru. Nimekuwa nikiweka pesa zangu katika benki yenu kwa muda wa miaka kumi na mitano mtawalia.

Kama ulivyosoma katika gazeti la tarehe 5.09.05, ninayo hamu kubwa ya kununua mkahawa uliotajwa. Tatizo linalonikabili ni kwamba pesa nilizo nazo kwa sasa hazitoshi. Hivyo naomba mkopo wa kiasi nilichotaja hapo juu ili niweze kununua mkahawa huo.

Meneja Mkurugenzi,
Kitale,
Benki ya Biashara,
Tawi la Kitale,
S.L.P. 24

6. Kwa kutumia maneno 150, eleza umuhimu wa biashara za kimataifa. (Alama 12)



Powered By: www.manyamfranchise.com